

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA



TANGAZO

ZABUNI YA KUVUNA MITI KATIKA MASHAMBA YA NYARUNAZI NA KANA KIGOMA VIJIJINI

ZABUNI NA: LGA/043/2018/2019/NC/01

TAREHE: 24/07/2019

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inakaribisha maombi kwa ajili ya kununua /kuvuna miti iliyopo katika mashamba ya miti ya Nyarunazi na Kana yaliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kilometa 35 – 40 njia kuu ya kwenda mpaka wa Tanzania na Burundi. Miti yote imekomaa na imefikia umri wa kuvunwa (*Rotation Age*); aina kuu ya miti iliyopo katika mashamba hayo ni:-

- (i) Mikaratusi (*Eucalyptus maidenii, Eucalyptus sidexylon & Eucalyptus saligna*),
- (ii) Misindano (*Pinus patella & Pinus radiata*), na

Maombi yaonyeshe bei ya kununua mti kulingana na aina ya miti, kipenyo chake (*diameter in cm*) au mita moja ya ujazo wa timbao (m^3) na idadi ya miti. Orodha ya aina ya miti, idadi yake, ukubwa (kipenyo) vimeainishwa katika jedwali Na. 1 hapo chini.

Jedwali Na. 1: Miti katika Msitu wa Nyarunazi na Kana

AINA (TREE SP.)	KIPENYO CHA MTI (DIAMETER IN CM AT DBH) NA IDADI YA MITI							JUMLA KUU	
	Less than 5cm	6 – 10 cm	11 – 20 cm	21 – 25 cm	26 – 30 cm	31 – 35 cm	Above 35 cm		
Misindano (Pinus SP)	11	1	-	38	58	108	167	383	MITI ILIYOPO KATIKA SHAMBA LA KANA
Misindano (Pinus patella, radiate)	60	-	-	-	-	-	-	60	
Mikaratusi (Eucalyptus spp)	1710	787	621	472	486	477	1353	6106	MITI ILIYOPO KATIKA SHAMBA LA NYARUNAZI
Misindano (Pinus patella, radiate)lusitanica)	6	7	40	110	166	106	169	604	

MASHARTI YA MWOMBAJI:

1. Mwombaji /Mnunuzi anaruhusiwa kwenda kuona shamba la miti analokusudia kuomba/kuvuna ili kufanya tathimini ya miti/mazao yaliyopo kabla ya kuomba zabuni.
2. Mwombaji/mnunuzi azingatie bei hallisi lliyopo ya soko la miti kwa sasa hivi.
3. Mwombaji/Mnunuzi anaruhusiwa kununua miti yote kama atakuwa na uwezo wa kununua zaidi ya aina moja.
4. Mnunuzi hataruhusiwa kuvuna miti mpaka awe amelipia malipo kamili.
5. Mnunuzi atalazimika kulipa fedha kulinganana idadi ya miti atakayokuwa ameshinda ndani ya siku saba (7) tangu kupewa tuzo la sivyo miti hiyo itauzwa kwa mnunuzi mwingine aliyeomba.
6. Mazao (mbao na mabanzi) baada ya kuvunwa yatatakiwa kulipiwa ushuru (cess) wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwa mujibu wa sheria .
7. Awe na leseni halali ya Biashara ya mazao ya misitu
8. Awe na TIN (Tax Identification Number)
9. Mwombaji awe na mashine ya kupasulia mbao
10. Mwombaji atatakiwa kukubaliana na maelekezo yoyote ya kitaalamu atakayopewa wakati wa kutekeleza zoezi la uvunaji na Mfumo wa uvunaji utakuwa ni kwa njia ya kuvuna miti yote (clear felling).
11. Waombaji ni lazima waonyeshe anuani zao kamili na mahali ofisi zao zilipo.
12. Mzabuni atakayeshinda, atatakiwa kulipia ushuru wa mazao ya misitu kadiri ya sheria na taratibu zilizowekwa kabla ya kusafirisha.(Kibali cha kusafirisha 'transit pass')
13. Mwombaji/mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kuvuna ndani ya siku 120.
14. Kabrasha la Zabuni linapatikana katika ofisi ya Katibu wa bodi ya Zabuni, Jumatatu hadi Ijumaa, Saa 1.30 Asubuhi hadi Saa 9.30 Alasili, isipokuwa siku za sikukuu/mapumziko. Ada ya kablasha la zabuni ni Tshs 30,000/= ilipwe kwa **DED-KIGOMA A/C Na. 51610000203** Nmb benki baada ya kuchukua hati ya malipo katika ofisi ya mapato. Baada ya malipo hayo mwombaji aje na stakabadhi ya benki (pay slip ili akatiwe risiti/stakabadhi atakayoambatisha kwenye kablasha lake la zabuni, aidha Ada ya maombi haitarudishwa.
15. Maombi yote yatumwe kwa: **KATIBU, BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA S .L .P. 332,KIGOMA**
16. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa wala kushughulikiwa.
17. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Jumatano tarehe 06/08/2019** saa 4.00 asubuhi na Zabuni zitafunguliwa saa 4.30 Asubuhi siku hiyo hiyo katika Ukumbi wa Halmashauri. Waombaji/Wawakilishi wanakaribishwa kushiriki ufunguzi.

P. Gwakila
PETRONILA B. GWAKILA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYAKIGOMA

